

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**CHUO CHA UALIMU BUTIMBA**

Anuani ya simu: 028-2552512  
Simu  
Fax:  
Email: butimbac@gmail.com  
**Unapojibu tafadhali taja:**



Chuo cha Ualimu Butimba,  
S.L.P. 1411,  
MWANZA:  
**TANZANIA:**

29/08/2018

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU  
WA MASOMO YA SAYANSI/FANI SEPTEMBER 2018/2019**

**1.0: UTANGULIZI: -**

Ninapenda kukuarifu kuwa umechaguliwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kujiunga na Mafunzo ya **STASHAHADA KATIKA MASOMO YA SAYANSI/FANI** katika chuo cha Ualimu Butimba. Chuo kinakupongeza kwa nafasi hii. Tunategemea kuwa utatumia nafasi hii vizuri katika masomo yako. Hivyo unatakiwa uwe na juhudi na moyo wa kujifunza darasani na nje ya darasa ili uweze kufaulu vizuri mafunzo yako.

**2.0: MAHALI CHUO KILIPO : -**

Chuo kipo mkoa wa Mwanza katika Halmashauri ya Nyamagana kilometa nane (08) kutoka mjini kati. Kuna njia kuu tatu za kukuwezesha kufika chuoni. Iwapo unatokea mjini kati panda daladala zilizoandikwa BUTIMBA TTC ambazo zitakufikisha hadi lango kuu la kuingia chuoni. Iwapo unatokea stendi kuu ya mabasi Nyegezi panda daladala zinazoelekea mjini na shukia Mkuyuni sokoni (Butimba Kona) au iwapo utatokea stendi ya kuu ya mabasi Buzuruga pia shukia Mkuyuni Sokoni (Butimba Kona) na hapo utapata usafiri mwingine wa daladala zitokazo mjini Mwanza kuja chuoni Butimba. Pia upo usafiri wa taxi kutoka hapo kona. Tusingeshauri sana usafiri wa bodaboda ambao pia unapatikana.

**3.0: TAREHE YA KURIPOTI: -**

Unatakiwa kufika Chuoni tarehe **04/10/2018** ili kuanza mafunzo na mwisho wa kuripoti ni tarehe **13/10/2018** baada ya hapo hutapokelewa kabisa.

### 3.1: USAJILI: -

Mwanachuo afikapo Chuoni, lazima aripoti kwa Msajili wa wanachuo kwa ajili ya kusajiliwa. Huruhusiwi kwenda Bwenini au maeneo mengine ya chuo kabla ya kupewa utaratibu toka Ofisi ya Usajili.

### 4.0: MUDA WA MAFUNZO: -

4.1 Kwa waliochaguliwa kusomea Stashahada ya Ualimu masomo ya Sayansi kwa sifa za kidato cha nne mafunzo yao yatakuwa ni kwa miaka mitatu (2018/2021)

4.2 Kwa waliochaguliwa kusomea Stashshada ya Ualimu masomo ya Fani kwa sifa za kidato cha sita, mafunzo yao ni kwa miaka miwili (2018/2020).

**NB.** Fani (somo mojawapo lenye ufaulu wa juu miongoni mwa yale uliyofanyia mtihani kidato cha sita pamoja na chaguo lako moja katika (muziki, sanaa za maonesho au elimu kwa michezo).

### 5.0: MAHITAJI YAKO BINAFSI: -

- Shuka jozi 2 za rangi ya bluu na mto wenye foronya ya bluu.
- Ndoo.
- Chandarua cha mbu.
- Daftari 8. (Counterbook quire two)
- Bukta ya bluu, fulana nyeupe na tracksuit ya blue.
- Raba nyeupe za michezo.
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
- Hati ya uthibitisho wa Daktari (imeambatanishwa).
- Scientific calculator kwa wanafuzi wa masomo ya sayansi
- Vifaa vya michezo, ala za muziki au maleba (mojawapo ya hivi kwa watakaokuwa wamechagua Fani).
- Lab coat jeupe (wanaosoma Sayansi).

### VYETI HALISI:

- Fika na **CHETI HALISI (Original Academic Certificate)** cha Kidato cha NNE kwa wahitimu wa kidato cha nne au cha NNE na cha SITA kwa waliohitimu kidato cha sita.
- Uje pia na **'Leaving Certificate'** yako ya shule uliyomalizia kidato cha Nne na cha Sita isipokuwa kama ulikua mtahiniwa wa kujitegemea (private candidate).
- USIPOKUJA NA VYETI TAJWA HAPO JUU, HUTAPOKELEWA CHUONI. **Tafadhali zingatia sana suala hili.**
- Kama wewe ni Mfanyakazi (mwajiriwa) njoo na kitambulisho chako halisi cha kazi na barua ya ruhusa kutoka kwa mwajiri wako.

## ADA YA CHUO:

Fedha ya **Ada** ya Chuo ni Tshs. **600,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani Tshs. **300,000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote Tshs. **600,000/=** kwa mara moja kwa mwaka.

Ada hii ya Chuo ilipwe kwa akaunti hii: **31101100057 [NMB]** Tawi lolote. Jina la akaunti ni **Butimba teachers college revenue.**

## MICHANGO MINGINE YA CHUO:

S/N	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo	5000	Mwaka
2	Huduma ya kwanza	5000	Mwaka
3	Usafi na miundombinu	20,000	Mwaka
4	Kukodisha godoro	20,000	Mwaka
5	Tahadhari	20,000	Kwa mwaka
6	Kitambulisho	5,000	Kwa mwaka wa kwanza
7	Michezo	10,000	Mwaka
8	Taaluma	50,000	Kwa mwaka
9	Usajili	5,000	Mara moja kwa mwaka wa kwanza
10	T-shirt yenye nembo ya chuo itapatikana chuoni	15,000	
11	TEHAMA/ICT	20,000	Mwaka
12	Ulinzi	15,000	Kwa mwaka
13	Kadi ya Bima ya Afya	50,400	Kwa wasio na kadi za Bima
	<b>JUMLA</b>	<b>240,400/=</b>	

**Nb:** 1. Utatakiwa kulipa ada ya mtihani wa taifa shilingi 50,000/= utakapokuwa mwaka wa wa mwisho (wa pili/tatu).

2. Mchango wa mahafali mtajulishwa kulingana na mahiaji.

Michango hii yote ambayo imeorodheshwa hapo juu (**240,400/=**) ilipwe kwenye akaunti ya michango ya Chuo **Na: 31101200023 [NMB]**. Jina la akaunti ni **Butimba teachers Training College.**

**ZINGATIA:** Ada na michango yote ilipwe katika akaunti namba na Benki elekezwa na siyo kupitia mitandao mingine.

## MUHIMU SANA:

Mwanachuo aje na **'Bank Pay in Slip'** au Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na **Stakabadhi/Pay in Slip** mbili, moja inayoonyesha malipo ya ada ya chuo na nyingine ionyeshe michango mingine ya chuo.

Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zioneshe jina kamili la mwanachuo husika. Ni vyema na wewe mwenyewe ukabaki na nakala ya hizo bank pay in slips.

### **VIFAA VINGINE KWA AJILI YA MATUMIZI YA CHUO :**

Kila mmoja aje na :

- i. Bunda (01) la karatasi (DOUBLE A, NOPA, SMART COPY).
- ii. Mfagio wa chelewa (01)
- iii. Mfagio soft broom (01)
- iv. Squeezer (02)
- v. Flat file (01)

### **6.0 SARE YA CHUO: -**


#### **A. Wanawake:**

- ❖ Sketi 2 nyeusi zenye kuvuka magoti sm 3 zikiwa na rinda moja tu, shati 2 light blue mikono mirefu na tai 2 ndefu (nyeusi), Viatu vyeusi visigino vifupi jozi 02 na soksi nyeupe jozi 02.
- ❖ Koti la suit rangi nyeusi (Ukiweza).

#### **B. Wanaume:**


- ❖ Suruali 2 (dark blue na nyeusi) zenye marinda, Shati 2 light blue mikono mirefu na tai 2 ndefu (rangi dark blue, viatu vyeusi 2 na soksi nyeupe jozi 02.
- ❖ Koti la suit rangi nyeusi (Ukiweza).

**NB:** Sare zote zinatakiwa kuwa na mshono ulioainishwa hapo chini katika picha namba 1 na namba 2 kwa wavulana na wasichana.



**PICHA Na. 2**

**Na.**



**PICHA  
1**

## **7.0 USAFIRI : -**

Unatakiwa ujigharimie mwenyewe kwa nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

## **8.0: CHAKULA : -**

8.1: Chuo kinatoa chakula kufuatana na uwezo wa serikali.

8.2: Chuo hakiruhusu wanachuo kujipikia mabwenini au mahali popote katika eneo la chuo. Hivyo USIJE NA SUFURIA AU JIKO LA KUPIKIA.

8.3: Chuo hakina chakula maalum (**special diet**) kwa wenye matatizo ya Afya au wenye Afya dhaifu ya kudumu.

## **9.0: MAWASILIANO:**

9.1: Mawasiliano yoyote yanayokuhusu wewe kutoka kwa ndugu zako au nyumbani **LAZIMA** yapitie kwenye uongozi wa Chuo, kwa Namba: (**0784623365** Mr. S R. Abdallah, M/Mkuu wa Chuo), **0755377668** (Mr. A. Ndomba, Msajili mkuu), (**0784563045** Mr. D. Mpama, Mwadili mkuu).

## **10.0: NIDHAMU**

Wakati wote uwapo hapa Chuoni unatakiwa kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi, mahali sahihi, na njia sahihi kwa mujibu wa **KANUNI/SHERIA** za chuo ambazo utazipata mara ufikapo Chuoni.

## **11: MWISHO: -**

Kila siku unategemewa kuwa mfano mzuri wa kuigwa na wanachuo wenzako, walezi na jamii kwa kutekeleza "**MOTTO**" wa Chuo "**JUHUDI NA MAARIFA**".

**KARIBU CHUO CHA UALIMU BUTIMBA**

**S. R. ABDALLAH  
K.N.Y MKUU WA CHUO**